**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**

**Simu ya shule Na. 0755297005/0787291765 Mkuu wa shule**

**0766591719 M/mkuu wa shule**
**E.MAIL. utawalataboraschool@gmail.com**
**SHULE YA SEKODARI TABORA WAVULANA,**
**S. L .P 374,**
**TABORA.**

**Kumb .Na. F.I/2020/1** **January, 2020.**

**Kwa**......................................................................
........................................................................

**YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2020**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza 2020 katika shule ya **wanafunzi wenye vipaji maalum** TABORA BOYS' SEC.SCHOOL. KARIBU SANA. Shule hii ni shule ya bweni ambayo masomo ya Sayansi ni ya lazima kwa wote. Shule itafunguliwa tarehe **06 January,2020.** Ni lazima ufike siku husika kabla ya saa 12:00 jioni na kupokelewa.

Shule iko umbali wa kilometa 3 kutoka stendi ya Mabasi na kilometa 2½ kutoka Railway Station.Utapokelewa shuleni utakapokuwa umetimiza mambo yaliyo kwenye viambatanisho **A – E.**

A: Maelezo Maalum
B: Sheria za Shule
C: Fomu ya Kujiandikisha
D: Fomu ya kuripoti ya kupimwa Hospitali
E: kivuli cha cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)

Ni matumaini yangu kuwa utasoma na kuzingatia maelezo yaliyotolewa. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule hii ya watoto wenye vipaji maalum ( **Special School** ).

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.............................................

DEOGRASIAS A. MWAMBUZI

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVULANA

Scanned by CamScanner

**KIAMBATANISHO A: MAELEZO MAALUM**

**1. SARE NA MAHITAJI YA BWENI**

Shule hii ni shule ya bweni hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuwa na mahitaji yafuatayo:

a) Suruali mbili za kaki, Suruali hizi zitapatikana Shuleni kwa bei ya Tsh. 20,000/ @ moja = 20,000 x 2= 40,000/= uamuzi huu wa kushonea suruali shuleni uliafikiwa na kikao cha wazazi kilichofanyika 30/08/2019 ili kuondoa utofauti unaojitokeza wa rangi na mishono.

b) Shati 2 au zaidi nyeupe tetroni mikono mifupi (aje nazo).

c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba viwe vya ngozi vyenye kisigino kifupi vinavyotumia (rangi ya viatu) kiwi nyeusi jozi moja au zaidi

**NB**: Awe na kandambili za kuogea

d) Jozi mbili au zaidi za soksi nyeupe.

e) Sweta la bluu, (v shape) lenye nembo ya shule linapatikana shuleni kwa bei ys Tsh. 13,000/=

f) Mkanda mweusi, usiwe na nembo au chuma kikubwa. Mikanda ya mabegi hairuhusiwi.

g) Aje na shuka mbili za pinki.

h) Nguo za michezo: Bukta ya Bluu, fulana ya bluu na viatu vya michezo (Aje navyo). Nguo hizi zisiwe na maandishi.

i) Truck suit, hizi zitapatikana shuleni zikiwa na nembo ya shule kwa Tsh 23,000/=

j) Mwanafunzi ajapo shuleni aje amevaa suruali nyeusi ya (Shamba dress) kitambaa yenye marinda mawili isiwe ya kubana mwili au mtepesho ( suruali hii itatumika mwanafunzi awapo nje ya darasa ndani ya Shule tu ) A naweza kuja nazo zaidi ya moja. Suruali za jinzi haziruhusiwi.

**NB;** Nguo za nyumbani tofauti na zilizotajwa hapo juu haziruhusiwi **akionekana nazo atafukuzwa shule mara moja.**

k) Mwanafunzi awe na "trunker" imara (sanduku la bati) ambalo litatumika kutunza vifaa vyake, vikiwemo vitabu na madaftari. Liwe na kufuli la kufungia.

l) Aje na ndoo moja 10Lts na kidumu cha lita tano cha kutunzia maji ya kunywa.

m) Kurunzi (Tochi) ya betri mbili. **Vifaa vya umeme haviruhusiwi kabisa.**

n) Aje na vifaa vya usafi binafsi kama mswaki n.k

o) Godoro 2½ x 6 lenye kitambaa (cover isiyofunguka).

p) Aje na Net (chandarua).



Scanned by CamScanner

q) Aje na vyombo vya chakula (sahani, kijiko,kikombe).

r) Ni lazima aje na bima ya afya, kama hana aje na Tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima ya mwaka mmoja. Shule haitahusika na matibabu ya mwanafunzi nje ya zahanati ya shule.

s) Aje na daftari kumi kubwa quire 4, daftari 10 quire 2 za mazoezi kwa kila somo, Mathematical set, kamusi ya Kiswahili na Oxford Dictionary maneno 25,000 na kuendelea, vitabu vya masomo yote tisa (History, Geography, English, Mathematics, Physics, Chemistry, Biology, Kiswahili na Civics)

t) Mwanafunzi aje na nakala ya Cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa.

**KIAMBATANISHO B: MAELEZO MAALUMU**

2:1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Pamoja na marekebisho yake yote.
Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni na muda wote wa maisha yako hapa shuleni.

**HESHIMA:**

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuiheshimu bendera ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.

**MAHUDHURIO:**

(a) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria darasani kila siku ya masomo na anawajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa. Ni marufuku kupiga kelele au kusumbua darasani na kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu. **Kutohudhuria darasani kutapelekea kufukuzwa Shule.**

(b) Mwanafunzi anapaswa ahudhurie paredi ya shule saa 12.00 jioni kila siku. **Kutohudhuria itapelekea kufukuzwa shule.**

(c) Mwanafunzi anapaswa kutii kengele ya shule kulingana na utaratibu au ratiba ya shule na dharura zinazojitokeza.

(d) Mwanafunzi anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za shule

(e) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi wa darasa/nyumba. Kosa la kukamatwa nje ya shule litapelekea kufukuzwa shule..

Scanned by CamScanner

**KIAMBATANISHO C: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA AHADI YA MZAZI KUKUBALIANA NA MASHARTI YA MWANAE KUJIUNGA NA SHULE HII**

1.Jina la Mwanafunzi.......................................................................................

2.Tarehe ya Kuzaliwa........................Mwezi:.......................Mwaka......

3.Amezaliwa katika Wilaya....................4.Uraia.............................

5.Shule anakotoka................................................................................

6.Mahali anapoishi kwa sasa.....................................................................

i) Wilaya......................., Tarafa................., Kata.............

Mtaa/Kijiji.........................................................................

7. Dini.........................................................................................................

8. Jina la Mzazi/Mlezi.............................. a) Kazi.......................

b) Anwani ya Mzazi/Mlezi.................................................

Mabadiliko yawasilishwe ofisini mara moja

c) Simu ya (Nyumbani/Mkononi)..............

9. Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya **DINI** yoyote.

Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Hivyo, kila siku ya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Aidha, kumepangiwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya Ijumaa na kila siku jioni dini baada ya chakula kuanzia Saa 1:00 – 1:45 usiku. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. **Mzazi amshauri mtoto vizuri kuzingatia agizo hili bila kuleta sababu zozote.**

10. Ahadi ya Mwanafunzi: Mimi...................................................

Ninakubali/Sikubali kutii kikamilifu kanuni, Sheria na maagizo ya shule yaliyotolewa hapo, kinyume cha hayo nikufukuzwa shule na ndiyo mwongozo wangu mpaka kumaliza Shule.

Saini ya Mwanafunzi:...............................................................

11.Ahadi ya Mzazi/Mlezi.............................................. Nakubaliana /Sikubaliani na maagizo yaliyotolewa hapo juu. Naahidi mwanangu akienda tofauti afukuzwe shule.

Jina la Mzazi/Mlezi: .................................. saini...........Tarehe:.........

| | | | |
|---|---|---|---|
| PICHA NA.1 | PICHA NA.2 | PICHA NA.3 | PICHA NA.4 |

Scanned by CamScanner

**2:2 B.MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA HATA KAMA NI KOSA LA KWANZA.**

i) Wizi ndani na nje ya shule.

ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

iii) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

iv) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

v) Kufuga ndevu.

vi) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

vii) Uvutaji wa sigara au bangi.

viii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

ix) Kugoma , kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa Shule.

x) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi pamoja na taratibu za shule.

xi) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule au vifaa vyovyote vinavyohusiana na simu kama **sim card na charger (SIMU HAIRUHUSIWI).**

xiv) Kudharau bendera ya Taifa.

xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

xvii) Kukataa adhabu halali toka kwa viongozi au walezi.

xviii) Kufanya/kushiriki udanganyifu kwenye mitihani ya ndani ya shule au nje.

NB: **MWANAO AKIBAINIKA KUTENDA MAKOSA / KOSA KATI YA HAYA ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**

Scanned by CamScanner

**SARE:**

(a) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule ya Tabora Wavulana wakati wote akiwa nje na ndani ya shule. Mwanafunzi anapaswa kuchomekea shati muda wote.

(b) Wakati usio kuwa wa masomo/darasani mwanafunzi anapaswa kuvaa suruali nyeusi pamoja na T Shirt yenye nembo ya shule/au ya blue. T shirt zenye nembo ya Shule zinapatikana Shuleni kwa Tsh. 15,000/=

(c) Wakati wa michezo, mwanafunzi anapaswa kuvaa bukta ya bluu na fulana ya blue na viatu vya michezo.

**UNADHIFU:**

(a) Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu
(b) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa chochote masikioni, shingoni wala mkononi isipokuwa saa.
(c) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na nywele ndefu au kunyoa mitindo au kuweka dawa nywele. Nywele ziwe na urefu wa kitana kidogo.
(d) Mwanafunzi anatakiwa kuwa nadhifu wakati wote awapo shule au awapo nje ya shule

**MAZINGIRA:**

(a) Kila mwanafunzi katika miaka yote hapa shuleni atatakiwa kupanda na kukuza mti mmoja wa kudumu
(b) Kila mwanafunzi atagawiwa eneo lake **maalum**(Special Area) ambalo atalitunza kwa usafi mpaka atakapomaliza shule
(c) Kila mwanafunzi atakuwa na zamu ya usafi katika Bwalo, Darasa, Vyoo na bweni.

**MAENEO YASIYORUHUSIWA KUFIKA MWANAFUNZI:**

(a) Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu.

i) Ofisi za Shule
ii) Bohari za Shule
iii) Maabara
iv) Jikoni
v) Baa, Kilabu au sehemu yoyote panapouzwa vileo na maeneo ya starehe
vi) Nyumba za wageni
vii) Nyumba za walezi bila sababu maalumu
viii) Kutoka nje ya eneo la shule baada ya saa 12:00 jioni bila ruhusa maalum.

**NB:** Ruhusa yoyote hutolewa kwa maandishi.

Scanned by CamScanner

**KIAMBATANISHO D:**
**STUDENTS MEDICAL CERTIFICATE "E"**

(To be completed by the Government Medical Officer and return to the Headmaster, Tabora Boys' Secondary School)

**Name:**..............................................................................

Please exam the student named above and comment in his health by responding to the following items. Kindly put a tick (√) in front of either **YES** or **NO** whichever is applicable.

| | | |
|---|---|---|
| A: **Sight?** If YES State | 1 NO | 2 YES |
| B: **Hearing:** If YES State | 1 NO | 2 YES |
| C: **T.B.** If YES State | 1 NO | 2 YES |
| D: **Blood Pressure** If YES State | 1 NO | 2 YES |
| E: **ASTHMA** | 1 NO | 2 YES |
| F: An other health problems | 1 NO | 2 YES |
| G: Any physical Disability? If YES State | 1 NO | 2 YES |

Do you therefore recommend the said student medically fit for studies.

Ship at this school?

1. NO
2. YES

If No please state:..........................................................................

Name and signature:..........................Designation:..........................

Date.......................................................

Official Stamp.............................................

Scanned by CamScanner

**KIAMBATANISHO E:**

**TABORA BOYS' SECONDARY SCHOOL**
**G. DAILY ROUTINE FOR STUDENTS**

| DAY | TIME | ACTIVITY |
|---|---|---|
| MONDAY | 05:30 AM – 06:45 AM | Cleanness |
| | 06:45 AM – 07:20 AM | Individual Parade |
| | 07:20 AM – 11:30 AM | Class Room |
| | 11:30 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12:00 PM – 02:40 PM | Classroom |
| | 02:40 PM – 03:20 PM | Lunch |
| | 03:30 PM – 05:00 PM | Afternoon Preparation |
| | 05:00 PM – 06:00 PM | Sports and Games |
| | 06:00 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 07:45 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Sleeping |
| TUESDAY | 05:30 AM – 06:45 AM | Cleanness |
| | 06:45 AM– 07:20 AM | Moring Parade |
| | 07:20 AM – 11:30 AM | Class Room |
| | 11:30 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12:00 PM – 02:40 PM | Classroom |
| | 02:40 PM – 04:20 PM | Lunch |
| | 03:30 PM – 05:00 PM | Afternoon Preparation |
| | 05:00 PM – 06:00 PM | Sports and Games |
| | 06:00 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Sleeping |
| WEDNESDAY | 05:30 AM – 06:45 AM | Cleanness |
| | 06:45 AM– 07:20 AM | Morning Parade |
| | 07:20 AM – 11:30 AM | Class Room |
| | 11:30 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12:00 PM – 02:40 PM | Classroom |
| | 02:40 PM – 04:20 PM | Lunch |
| | 03:30 PM – 05:00 PM | Afternoon Preparation |
| | 05:00 PM – 06:00 PM | Sports and Games |
| | 06:00 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Sleeping |
| | 05:30 AM – 06:45 AM | Cleanness |
| | 06:45AM – 07:30 AM | Individual Preparation |
| | 07:00 AM – 07:30AM | Morning Parade |
| | 07:30AM – 11:30 AM | Class Room |

Scanned by CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| THURSDAY | 11:30 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12:00 PM – 02:40 PM | Classroom |
| | 02:40 PM – 04:20 PM | Lunch |
| | 03:30 PM – 05:00 PM | Afternoon Preparation |
| | 05:00 PM – 06:00 PM | Sports and Games |
| | 06:00 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Seeping |
| FRIDAY | 05:30 AM – 06:45 AM | Cleanness |
| | 06:45AM – 07:30 AM | Morning Parade |
| | 07:30 AM– 11:30 AM | Class Room |
| | 11:30 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12:00 PM – 02:40 PM | Religion (Muslim) |
| | 02:40 PM – 04:20 PM | Lunch |
| | 03:30 PM – 05:00 PM | Evening Preparation |
| | 05:00 PM – 06:00 PM | Sports and Games |
| | 06:00 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Sleeping |
| SATURDAY | 05:30 AM – 07:00 AM | Morning Jogging |
| | 07:00 AM – 01:00 PM | Worship sabath |
| | 07:00 AM – 09:00 AM | Cleanness |
| | 09:00 AM – 11:30 AM | Private Study |
| | 11:00 AM – 12:00 PM | Break |
| | 12.00PM - 02:00 PM | Private study |
| | 02:00 PM – 02:40 PM | Lunch |
| | 02:40 PM – 05:45 PM | Personal Cleanness |
| | 05:45 PM – 06:30 PM | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 05:30 AM | Sleeping |
| SUNDAY | 07:00 AM – 01:00 PM | Sunday Worship. |
| | 01:00 PM – 02:40 PM | Lunch |
| | 02:40 PM – 05:45 PM | Personal Cleanness |
| | 05:45 Pm – 06:00 Pm | Evening Parade |
| | 06:30 PM – 07:00 PM | Dinner |
| | 07:00 PM – 08:00 PM | Religion |
| | 08:00 PM – 11:00 PM | Night Preparation |
| | 11:00 PM – 5:30 AM | Sleeping |

DEOGRASIAS A. MWAMBUZI

**Mkuu wa shule**

WA SHULE

TABORA WAVULANA



Scanned by CamScanner